



USAID

KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



Wanafunzi wa Sekondari katika Wilaya ya Karatu.

Picha na: Rachel Chilton/USAID

TANZANIA **WAACHE WASOME**

Waache Wasome ni mradi wa miaka mitano ambao unakusudia kuongeza ushiriki na kuhakikisha wasichana walio katika rika balehe wanabakia shulenii katika shule za sekondari.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuongeza viwango vya ushiriki wa wasichana kwa shule za sekondari. Walakini, wakati idadi kubwa ya wavulana na wasichana inaanza kidato cha kwanza kila mwaka, mwisho wa miaka minne, wasichana wengi hawatakuwa tena shulenii. Jitihada za Waache Wasome zimebekwa katika misingi ya kuwawezesha wasichana kuunda na kufikia malengo kwa mustakabali wa maisha yao, wakati wa kushughulikia masuala ya kijamii / jinsia, vizuizi vya kiuchumi, na uktili vinavyozuia uwezo wao wa kubaki na kufanikiwa shulenii.

Malengo ya Waache Wasome ni:

1. Kujenga uwezo, maarifa, na mbinu za kuwakinga wasichana wa shule za sekondari
2. Kuongeza kujitolea kwa familia na uwezo wa kuwekeza katika elimu ya watoto wa kike
3. Kuzingatia mazingira rafiki ya shule kwa watoto wa kike.
4. Kutoa njia mbadala za masomo kwa watoto wa kike ambao wameacha shule za sekondari kwa sababu ya ujauzito na / au ndoa

Waache Wasome inafanya kazi kwa karibu na viongozi wa serikali za mitaa, uongozi wa shule, waalimu, viongozi wa jamii, na wazazi kuleta mpango kamili wa ushirikiano kwa halmashauri inayolengwa na kuhakikisha umiliki wa mradi katika ngazi ya mitaa. Mradi huo pia utafanya kazi na vyombo vya serikali kusaidia usambazaji na utekelezaji wa sera zinazohusu wasichana wa rika balehe.

MATARAJIO YA MRADI

Ushiriki wa Waache Wasome umetengenezwa sambamba na vipaumbele vyaya sera ya elimu na mafunzo ya Tanzania ya mwaka 2014, Sheria ya Watoto ya mwaka 2009, na mpango wa kitaifa wa kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Kwa mwaka wa kwanza, mradi ulishiriki katika shule sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, kwa kiwango cha hadi shule 105. Mradi utafikia shule 105 na takribani vijiji 268 kufikia mwaka wa tano katika halmashauri nne.

- Kuzifadhili shule kuandaa klubu za Protect Our Youth (Linda Vijana Wetu) ambazo zinakuza mabadiliko kwa vijana wa rika balehe kwa kuwawezesha kwa habari, ustadi, ili waweze kutambua vizuri aina ya hatari zinazowakabili na kujenga uwezo wa kuwa na kinga dhidi ya hatari hizi.
- Kuunda vikundi vyaya "Uboreshaji wa Maisha kwa akina mama na walezi wa Vijana", ambavyo vinasaidia mabadiliko katika kiwango cha kaya vilivyoundwa kusaidia mama na walezi na kutoa msaada zaidi kwa kuhakikisha watoto wa kike wanaendelea na masomo.
- Kutoa mafunzo ya walimu na wasimamizi wa shule ambayo huwafanya kuwa na maarifa na ustadi wa kuzuia na kupambana na ukatili wowote wa kijinsia shulen, kukuza uhusiano mzuri na wanafunzi, na kupambana na changamoto zinazochangwa na mila na desturi.
- Kuanzisha vikundi vyaya masomo vyaya nje ya-shule, ambavyo vinatoa msaada kwa wasichana walio katika mazingira hatarishi ambao wameacha shule. Hivi husaidia vijana ambao ni mamawazazi kufanya maamuzi bora, kukuza uwezo wa kujiamini, na kupunguza mazingira hatarishi yanayoweza kuepelekea kupata maambukizi ya VVU.

BAJETI Dola za Marekani milioni 14.75

MUDA

Disemba 2016 – Februari 2022

MAEneo YA MRADI

- Halmashauri ya Wilaya ya Karatu
- Halmashauri ya Wilaya ya Musoma
- Halmashauri ya Manispaa ya Musoma
- Halmashauri ya Wilaya ya Tarime

MTEKELEZAJI

World Education Inc, Bantwana Initiative
<https://bantwana.org/>

MSHIRIKA

Serikali ya Tanzania
NORC at the University of Chicago
WGBH Educational Foundation

MAWASILIANO YA USAID

Aaron Miles
Afisa Mwakilishi wa Mradi (AOR)
+255 746 700 858
amiles@usaid.gov

MAWASILIANO YA MTEKELEZAJI

Lilian Badi
Mkuu wa Mradi
World Education, Inc.
+255 272 545 525
Lilian_badi@tz.worlded.org

KWA TAARIFA ZAIDI

Tovuti: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania